

Kwa Nini Wakristo Walioanguka Hukataa Kumrudia Bwana?

Agano Jipya huwaonya waziwazi wakristo kuhusiana na ukengeufu. Yesu anaeleza kwamba yeye aangaliaye nyuma huku akilima hafai katika ufalme wa Mungu, Luka 9:62. Petro naye katika Waraka wake wa pili mlango wa pili, anatabiri kuhusiana na ujio wa walimu wa uongo watakaoleta ukengeufu wenye uharibifu.

Anatangaza na adhabu fulani kwa wale wanaoanguka kutoka kwa Mungu. Na anatuhadharisha na sisi kwamba wale wanaoanguka kutoka kwenye neema ni heri wasingelimjua Bwana, 2 Petro 2:20-22. Tunajua kuwa kuanguka kutoka kwenye neema ni hatari mno kwa roho zetu. Lakini, kwa nini wengine wanaanguka hawaioni njia ya kurudi nyumbani? Wengine wanashindwa kuiona njia ya kwenda nyumbani kwa Mungu kwa sababu:

Wanaupenda uongo kuliko kuipenda kweli.

_Ni dhahiri kwamba hakuna mkweli duniani kuliko injili ya Yesu Kristo isiyoghoshiwa. Na tukizingatia mafundisho yake tutafanya vema, 2 Petro 1:19. Ingawaje mafundisho yake ya upendo, neema, msamaha na rehema ni ukweli mwepesi ambao kila mwana wa Mungu anatakiwa kuufurahia. Ukweli ni kwamba shetani amepata nafasi ya kuutwaa msingi wa ukweli huu na kuugeuza kuwa uongo. Uongo kwa ujumla, neema pekee yake, imani pekee yake na matendo pekee yake. Uongo ambao unaingia waziwazi na kufariji, lakini hauwi umejikita katika Neno la Mungu. Kwa hiyo baadhi ya wakristo walioanguka hawatarudi nyumbani kwa sababu wanakuwa wamepata mafundisho ambayo yanawapendeza zaidi katika roho zao. Tunakiwa kuwatahadharisha kwamba hukumu ya milele inawasubiri wanaoipokea injili nyingine ambayo haijaletwa na Kristo kwa njia ya Roho Mtakatifu, Wagalatia 1:6-9.

Wanaipenda dhambi kuliko kuipenda kweli-

_Paulo anaweka tofauti kubwa baina ya kuenenda katika Roho na kuenenda katika mwili katika Wagalatia 5:16-26. Paulo, kwa njia ya Roho Mtakatifu anaeleza waziwazi kwamba wale wanaoenenda katika mwili hawataurithi ufalme wa Mungu. Shetani ameifungasha dhambi kama kifurushi cha kutamanika ambacho mtu anaweza kumwacha Kristo kwa ajili ya matendo ya Mwili. Hivyo, wapo wakristo wengi walioanguka ambao watakataa kumrudia Bwana kwa sababu wana mapenzi mapya, mwili.

Wanapenda familia kuliko kuipenda kweli;

Yesu alisema katika Mathayo 10:36, “na adui za mtu ni wale wa nyumbani mwake” Kuna namna nyingi za familia, lakini jambo lililo la hakika ni kwamba tunatakiwa kumpenda Mungu kuliko wanandugu, Luka 14:26. Wakristo wengi sana wameanguka kwa sababu walikuwa wametingwa kuzifukuzia ndoto kama mpira wa kikapu, kuwinda, magari na mashamba na matukio ya kifamilia. Wengine wameanguka kwa sababu mwenzasiye mkristo ameuliza kuwa “kwa nini unanipenda kidogo?” Naye mkristo ili kumthibitishia upendo, anaacha kuhudhuria ibada, ibada moja moja hadi walipoachana na Mungu wao. Tunachotakiwa kukumbuka ni kuwa upendo mkuu tunaoweza kuwa nao katika familia zetu ni kuwa waaminifu kwa Mungu, 1 Wakorintho 7:14.